



Katika

# Matunda ya Taqwa

**Sh. Mohammad ibn  
Saalih al-'Uthaimeen  
(rahimahullah)**

*Katika*

# *Matunda ya Takwa*

na

**Shaykh Muhammad ibn Saalih  
al-'Uthaimen**

Imefasiriwa na

Abu Malaadh Sa'eed Baadel al-Hadhramee

Uk. 1

Sifa zote njema ni zenye kumthubutukia Allah, Mola wa ulimwengu. Na swala Zake na salamu zimfikie Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Muhammad Sallallahu Alaihi Wasalam, na jamii yake, maswahaba na wale waloufuata uongofu wake hadi siku ya Kiyama.

Enyi ndugu mulioamini!

Ama kweli nasiha aliowapa Mwenyezi Mungu Alietukuka waja Wake kutoka zama za Adam mpaka zama hizi, ni kuwa na taqwa (ucha Mngu), Utukufu na Ukubwa ni Wake Yeye.

Alie na Nguvu na Ufalme amesema,

Na kwa hakika tuliwausia walio pewa Kitabu kabla yenu, na

وَلَقَدْ وَصَّيْنَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ  
مِنْ قَبْلِكُمْ وَإِيَّاكُمْ أَنْ اتَّقُوا اللَّهَ وَإِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ  
مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ غَنِيًّا حَمِيدًا

nyinyi pia, kwamba muwe na taqwa (mumche Mwenyezi Mungu). Lakini mukikufuru, basi ni vya Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo duniani. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitosha, na Msifiwa." <sup>1, 2</sup>

Nayo pia ni nasiha ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu Sallallahu Alaihi Wasalam kwa ummah wake:

Abee Umaamah Suddee ibn 'Ujlaan al-Baahilee, radhiallahu anhu amesema: Nilimsikia Mtume Sallallahu Alaihi Wasalam akitoa khutba siku ya Hajj yake ya mwisho, akasema, "Mcheni Mola wenu, salini salat zenu tano, fungeni mwezi wa

---

<sup>1</sup> Soorah an-Nisaa' 4:131

<sup>2</sup> Al-Haafidh Ibn Katheer amesema kuwa "Mwenyezi Mungu amekuamrisheni nyinyi kama alivyowaamrisha wale kabla yenu ili kumcha Yeye pekee na sio yeyote mwengine". Tafseer Qur'an al-'Adheem (1/504)

Ramadhan, lipeni Zakat, na muwatii viongozi wenu, mutakapo fanya hivo, mutaingia Pepo ya Mola wenu".<sup>3</sup>

Kila wakati Mtume Sallallahu Alaihi Wasalam anapomtuma kiongozi wa vita katika msafara wa kijeshi, alimnasihi awe na taqwa ya dhati juu ya Mwenyezi Mungu, na aliwanasihi na wanajeshi hali kadhalika.

Watangulizi wetu wema (salaf) hawakuacha kupeana nasiha juu ya taqwa ya Mwenyezi Mungu katika hotuba zao, katika barua zao, na katika kushuhidia kwao kwa jambo baada ya kufariki kwa Mtume Sallallahu Alaihi Wasalam.

'Umar ibn al-Khattab radhiyallahu anhu alimwandikia mtoto wake 'Abdullah: " Kutangulia: Nakunasihhi uwe na taqwa ya Allah Mwenye Nguvu zote, Mwenye Ufalme, kwani yeyote mwenye kumcha Yeye, Allah humhifadhi, na yeyote mwenye kumkopesha Mwenyezi Mungu, Allah humjazi, na yeyote mwenye kumshukuru, Mwenyezi Mungu humzidishia."

'Alee radhiyallahu anhu alimpa nasaha mtu mmoja, na kumwambia: "Nakunasihhi uwe na taqwa ya Allah Mwenye Nguvu zote na Ufalme. Hamna kuumbaa na kukutana Naye na hamna mwengine wa kukutana nawe ila Yeye unapofika siku ya Kiyama, kwani hakika Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kumiliki dunia hii na kesho siku ya Kiyama."

Mmoja katika watu wema alimwandikia nduguye Muislamu: "Nakunasihhi kuwa na taqwa ya Allah ambaye anajua siri zako na anaona vitendo vyako vya wazi, mkumbuke Mwenyezi Mungu kila wakati wa usiku na mchana, na umche kutokamana na ukaribu Wake, na nguvu Alizonazo kwayo. Na utambue kuwa daima Anakutazama. Na usiwache maamrishi yake na kufuata maamrishi mengine, wala milki Yake na kutaka milki nyengineo, basi mtukuze Yeye kwa kumcha kwa wingi."

Maana ya taqwa ni kuwa, mja anaweka kati yake na kile anacho kiogopa, ngao itakayo mlinda.<sup>4</sup>

---

<sup>3</sup> Imepokewa na at-Tirmidhee

Maana ya taqwa kuhusu waja wa Mwenyezi Mungu Alietukuka ni " Mja anaweka baina yake na kile anachokihofia yaani - kupata hasira na laana ya Mola wake - ngao ambao itamlinda." Kwa kumtiii Yeye na kujiepusha na kum'asi.

Ndugu yangu mhashimiwa, yanayo fuatia ni baadhi ya misemo kutoka kwa watangulizi wetu wema (ma salaf), katika kueleza maana ya taqwa ya Allah:

Ibn 'Abbaas radhiallahu anhu amesema: " Wale wanaomcha Mwenyezi Mungu ni wale wanaomjali Allah na adhabu zake."

Taabi'ee Talq ibn Habeeb <sup>5</sup> amesema: " Iwapo jambo baya litakufikieni, izimisheni na taqwa." Alipoulizwa taqwaa ni nini, akajibu: "Taqwa ni kule kufanya vitendo kwa kumtiii Mwenyezi Mungu Alietukuka, na kutarajia Rehema Zake, juu ya mwangaa kutoka Kwake; na taqwa ni kuwacha vitendo vya kum'asi Mwenyezi Mungu Alietukuka kutokana na kumwogopa, juu ya mwangaa kutoka Kwake." <sup>6</sup>

Ibn Mas'ood radhiallahu anhu amesema: "Kusema kuhusu neno la Mwenyezi Mungu Alietukuka,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ

Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu <sup>7</sup>

---

<sup>4</sup> Ibn Rajab rahimahullah amesema: "Asili ya taqwa nikuweka ngao kukulinda na ghadhabu za Mwenyezi Mungu na adhabu Yake. Ngao hio ni kufuata maarisho Yake na kujikinga na yale Alioyakataza..." (Jaami' ul-'Uloom wal Hikaam: 190/191).

<sup>5</sup> Talq ibn Habeeb alikuwa ni taabi'ee mashuhuri. Alitambulika kwa ilmu yake, ucha Mngu wake na kisomo chake cha Qur'an.

<sup>6</sup> Imepokewa na Ibn Abee Shaybah katika Kitaabul-Eemaan Na. 99 na imesahihishwa na Shaykh al-Albanee.

<sup>7</sup> Soorah al-'Imraan 3:102

Nikuwa Mwenyezi Mungu Alietukuka anatakiwa kutiwa, wala asiwe ni mwenye kuasiwa; Akumbukwe kila wakati, wala kutosahauliwa; na atakiwe shukrani, na wala tusiwe ni wenye kumtoa shukrani."

Kwa hivyo jipinde ewe ndugu yangu mheshimiwa, katika kumcha Mwenyezi Mungu, alie na Nguvu zote na Utukufu, kwani Yeye, sifa zote zimfikiye, anastahiki kuogopwa, kuwa stahi, na kutukuzwa ndani ya moyo wako.

Yafuatayo ni baadhi ya manufaa yaliowazi, yanayotokamana na kumcha Mwenyezi Mungu Alietukuka katika dunia hii:

### **1 - Hakika, kumcha Mwenyezi Mungu Alietukuka kunasababisha majambo yote ya mwanadamu kuwa mepesi.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema:

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مِنْ أَمْرِهِ يُسْرًا ﴿٤﴾

Na anaye mcha Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu humfanyia mambo yake kuwa mepesi <sup>8</sup>

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ ﴿٥﴾ وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿٦﴾ فَسَنِّيْسِرُهُۥ لِلْيُسْرَىٰ ﴿٧﴾

Ama mwenye kutoa (katika Sadaqa) na akamcha Mungu, Na akaafiki al-husnaa (malipo mema kutoka kwa Allah) Tutamsahilishia yawe mepesi. <sup>9</sup>

---

<sup>8</sup> Soorah at-Talaaq 65:4

<sup>9</sup> Soorah al-Layl 92:5-7

## 2 - Taqwa inamlinda mwanadamu na madhara ya shaytaan.

إِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا إِذَا مَسَّهُمْ طَئِيفٌ مِّنَ الشَّيْطَانِ تَذَكَّرُوا  
فَإِذَا هُمْ مُبْصِرُونَ ﴿٢٠١﴾

Hakika ya wale walio na taqwa ya Allah, wakati uchochezi wa shaytaan unapowajia, wanamkumbuka Mwenyezi Mungu na hakika tayari wanaona (kila kitu kuwa sawa).<sup>10</sup>

## 3- Kwa hakika, taqwa pia ni sababu ya kufunguliwa kwao kwa rehma kutoka mbinguni na katika ardhi.

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ  
مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

Na lau kuwa watu wa miji wangeli amini na wakawa na taqwa, kwa yakini tungeli wafungulia baraka kutoka mbinguni na katika ardhi.<sup>11</sup>

## 4 - Taqwa inamfanya mja wa Mwenyezi Mungu kufaulu katika kutofautisha baina ya haki na baatil (kosa), na kuwa na ilimu ya kila mojawo.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَل لَّكُمْ فُرْقَانًا

Enyi mlio amini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atakupeni furqaan (kipambanuo cha kujua baina ya sawa na makosa)

<sup>12</sup>, <sup>13</sup>

---

<sup>10</sup> Soorah al-A'raaf 7:201

<sup>11</sup> Soorah al-A'raaf 7:96

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ  
 وَعَآمِنُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِن رَّحْمَتِهِ وَيَجْعَلْ لَكُمْ  
 نُورًا تَمْشُونَ بِهِ

Enyi mlio amini! Kuweni na taqwa ya Allah, na muaminini Mtume wake, atakupeni sehemu mbili katika Rehma Yake, na atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo.<sup>14</sup>

---

<sup>12</sup> Soorah al-Anfaal 8:29

<sup>13</sup> Al-Haafidh Ibn Katheer (d. 777H) rahimahullah amesema: "Ibn Abbaas, as-Sudee, 'Ikramah, ad-Dahhak, Qataadah na Muqaatil Ibn Huyyaan, wote walisema kuhusu "Furqaan" kuwa inamaanisha njia ya kutoka (na matatizo). Mujaahid akaongeza: Njia yakujitoa (na matatizo) katika dunia na kesho akhera. Katika riwaya kutoka kwa Ibn Abbaas kuwa amesema inamaanisha "uwokovu"; na katika riwaya nyengine kutoka kwake: "kusaidiwa". Muhammad Ishaq amesema kuwa inamaanisha: kipambanuo cha kutambua baina ya sawa na makosa. Elezo huu wa Ishaq ndio uliowastani zaidi kulingana na yale yaliotangulia na ndio matokeo halisi ya hayo. Kwani yeyote mwenye taqwa ya Allah kwa kutii maamrishi Yake na kuepukana na makatazo Yake, atapewa uwezo wa kutambua kilicho sawa na makosa. Na hii ndio itakuwa sababu yake ya uwokovu, kusaidiwa, na sababu ya mambo yake ya kilimwengu kuwa mepesi na furaha yake siku ya Kiyama. Itakuwa ndio sababu ya dhambi zake kusamehewa na Mwenyezi Mungu Alietukuka, na yeye kupawa msamaha na Mwenyezi Mungu Alietukuka kumlinda na watu. Na itakuwa vile vile sababu yake kupata malipo makubwa kutoka Mwenyezi Mungu Alietukuka; kwani amesema Mwenyezi Mungu Alietukuka "**Enyi mlio amini! Kuweni na taqwa ya Allah, na muaminini Mtume wake, atakupeni sehemu mbili katika Rehma Yake, na atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo.**" [Qur'aan Soorah al-Hadeed 57:28] Tafseer Qur'aan al-'Adheem (2/301-302) ya Ibn Katheer.

<sup>14</sup> Soorah al-Hadeed 57:28



**5 - Iwapo Muumini atapitikana ni matatizo, hakika kuwa na taqwa itamwezesha kutoka kwenye matatizo hayo, na kupata maandao na mepesi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Alietukuka, mifano ambao asingeweza kudhania.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema,

بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ﴿٢﴾ وَيَرْزُقْهُ  
مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ

Na mwenyekuwa na taqwa ya Allah, Mwenyezi Mungu humfungulia yeye njia ya kutokoea (matatizo). Na anamruzuku kwa njia asizodhania. <sup>15</sup>

**6 - Kwa hakika taqwa ni njia ya kupata kuwa muangalizi wa dini ya Mwenyezi Mungu. Kwani, waangalizi wa dini ya Mwenyezi Mungu bila shaka ni wale wanaomcha.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema,

إِنَّ أَوْلِيَاءُؤُهُ إِلَّا الْمُتَّقُونَ

Hawakuwa walenzi Wake Ila ni muttaqoon. <sup>16, 17</sup>

وَإِنَّ الظَّالِمِينَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُتَّقِينَ ﴿١٦﴾

---

<sup>15</sup> Soorah at-Talaaq 65:2-3

<sup>16</sup> Soorah al-Anfaal 8:34

<sup>17</sup> Muttaqoon inamaanisha: "wale wenye taqwa" yaani mtu mchaMungu, mwenye kutenda mema, kumwogopa na kumpenda Allah, na wala wanaojihadhari sana katika kutomkasirisha.

Na hakika wenye kudhulumu ni marafiki na walenzi wao kwa wao. Na Mwenyezi Mungu ni rafiki na Mlinzi wa muttaqeen (wanaomcha na kutenda mema).<sup>18</sup>

**7 - Taqwa inamwezesha Muumini kutohofia shari lolote linalosababishwa na makafiri wasioamini au na njama zao.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَإِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا لَا يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا  
إِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ

Na nyinyi mkisubiri na mukawa na taqwa, hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kuyazunguka yote wayatendayo.<sup>19</sup>

**8 - Pia ni sababu ya Mwenyezi Mungu Alietukuka kuteremsha usaidizi wakati wa tatizo, na kukutana na maadui wa Mwenyezi Mungu.**

Amesema mwenyezi Mungu Alietukuka

---

<sup>18</sup> Soorah al-Jaathiyah 45:19

<sup>19</sup> Soorah al-'Imraan 3:120

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرِ وَأَنْتُمْ  
 أَذِلَّةٌ فَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢٣﴾ إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ  
 أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ يُبَدِّدَ كُمْ رَبُّكُمْ بِثَلَاثَةِ آلَافٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ  
 مُنزَلِينَ ﴿١٢٤﴾ بَلَىٰ إِن تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا وَيَأْتُوكُم مِّن فَوْرِهِمْ هَذَا  
 يُبَدِّدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ آلَافٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُسَوِّمِينَ ﴿١٢٥﴾ وَمَا جَعَلَهُ  
 اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوبُكُم بِهِ ۗ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ  
 الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿١٢٦﴾

Na Mwenyezi Mungu alikwisha kunusuruni katika vita vya Badri nanyi mlikuwa wanyonge. Basi kuweni na taqwa ya Allah ili mpate kushukuru. . Kunbuka (ewe Muhammad) ulipo waambia Waumini: “Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu walio teremshwa?” Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkawa na taqwa ya Allah na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanao wenye alama (za tuzo za ushindi). Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipo kuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliye tukuka, Mwenye nguvu na Mwenye hikima. <sup>20</sup>

Kuteremshwa kwa msaada unakuwa ndio bishara njema kwa waumini, utulivu wa moyo na tuzo la usidizi kutoka kwa Aliye Na Nguvu, Mwenye Hikma.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوبُكُم بِهِ ۗ وَمَا  
 النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿١٢٦﴾

<sup>20</sup> Soorah al-Imraan 3: 123-126

Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipo kuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliye tukuka, Mwenye nguvu na Mwenye hikima.<sup>21</sup>

## **9 – Taqwa inafanya kutokuwepo na chuki au hasira baina ya waja wa Mwenyezi Mungu.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

Na saidianeni katika al-birr na at-taqwa (kufanya wema na uchamngu). Wala msaidianeni katika dhambi na uadui.<sup>22, 23</sup>

Mwenyezi Mungu ametaja katika kisa cha Maryam

---

<sup>21</sup> Soorah al-Imraan 3:126

<sup>22</sup> Soorah al-Maaidah 5:2

<sup>23</sup> *Birr* ni ubora wa wema na zuri inalopatikana katika kitu. Hii ndio inayotokamana na kiini cha neno hili katika lugha ya Kiarabu. Iliolingana nayo ni *burr* (ngano) ambayo inamanufaa kuliko nafaka zenginezo katika umanufaa na uzuri. Pia, mtu mzuri anaitwa *barr* (anayetekeleza ahadi). Mwenyezi Mungu amewataja malikah kuwa ni *Bararah* (wema na waadilifu) na wakazi wa peponi kuwa ni *abraar* (wema). *Birr*, kwa hivyo inakusanya vitu vyote vizuri na vikamilifu vinavyopatikana katika binadamu. Tofauti yake ni *ithm* (dhambi). An-Nuwaas bin Si'maan radhiallahu anhu ametunukulia kuwa Mtume Sallallahu Alahi Wasallam amesema: “*Birr* ni tabiya nzuri, na *ithm* ni yale fikra (ovu) yanayo pita katika kifua chako na unahofia kuwa watu wengine watayajua. [Imepokewa na Muslim]

Taqwaa kwa upande mwingine, ni njia zinazo ongoza kwa *birr*. Kiini cha neno hili katika lugha ya Kiarabu inamaanisha “kinga”. Mtu anayetekeleza jambo hili anajikinga na adhabu ya moto. Kwa hivyo nasaba ya *birr* na *taqwa* ni sawa na kusema afya (ambayo ndio kusudio) na hifadhi ya mwili (ambayo ndio njia ya kutekeleza).

فَأَرْسَلْنَا إِلَيْهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا ﴿١٧﴾ قَالَتْ  
 إِنَّيَأَعُوذُ بِالرَّحْمَنِ مِنْكَ إِن كُنْتَ تَقِيًّا ﴿١٨﴾

Tukampelekea Roho wetu (Jibrael), akamtokelea kwa njia sawa na mtu. (Maryam) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema aniepushe nawe, (hivyo basi niache) ikiwa wewe ni mchamngu.<sup>24</sup>

## 10 – Taqwa inamfanya Muumini kuyatukuza ishara za Mwenyezi Mungu (sehemu tukufu)

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

ذَلِكَ وَمَنْ يُعْظِمْ شَعْتِيرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٣٣﴾

Hivyo basi, yeyote anayetukuza ishara za Mwenyezi Mungu, hayo ni katika taqwa ya moyo (unyenyekavu wa moyo).<sup>25</sup>

## 11 – Na ndio njia Muumini anafanya matendo mema, na ndio sababu ya hayo matendo kukubaliwa na Mwenyezi Mungu. Vile vile ndio njia ya kusamehewa dhambi.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

يَتَابُهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْتَفُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُصْلِحْ  
 لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ  
 فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾

Enyi Mulioamini! Kuweni na taqwa ya Allah na semeni ukweli. Atawaongozeni katika kufanya mema na vitendo vya sawa na kuwasameheni dhambi zenu na yeyote mwenye

<sup>24</sup> Soorah Maryam 19: 17-18

<sup>25</sup> Soorah al-Hajj 22: 32

kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa hakika amefanikiwa mafanikio makubwa mno. <sup>26 27</sup>

**12 – Taqwa inamfanya Muumini kuteremsha sauti yake mbele ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu Sallallahu alaihi Wasallam, iwe ni katik auhai wake au baada ya kifo chake.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

إِنَّ الَّذِينَ  
يَعُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ  
قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَى لَهُم مَّغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٣﴾

Kwa hakika wanao teremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezipa mtihani nyoyo zao na taqwa. Kwao ni maghfira na ujira mkubwa. <sup>28</sup>

Wanavyuoni wamesema: Haipendekezwi kuenuwa sauti mbele ya kaburi la Mtume Sallallahu Alaihi Wasalam kama ilivyochukizwa kuenua sauti mbele yake alipokuwa hai. Vile alivyo heshimiwa alipokuwa hai ndivo ahishimiwe anapokuwa kaburini mwake.

**13 – Taqwa inamfanya Muumini kupata Mapenzi ya Allah, na haya Mapenzi ambayo Mwenyezi Mungu anayoweka juu ya Muumin ni ya maisha haya ya leo na ya kesho siku ya akhera.**

Mtume Sallallahu Alaihi Wasallam amesema kuwa Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema: " Hamna njia iliobora zaidi ambayo mja wangu anakuja karibu Nami, ila kwa kupitia

---

<sup>26</sup> Soorah al-Ahzaab 33: 70-71

<sup>27</sup> Soorah al-Ahzaab 33: 70-71

<sup>28</sup> Soorah al-Hujuraat 49: 3

vitu ambazo nimemfanyia kuwa ni wajibu kutekeleza. Na waja wangu wanaotekeleza yale mambo ya Sunnah, wanakaribia zaidi, mpaka ninampenda, na Nikimpenda, Ninakuwa ndio masikio yake ambayo anayatumia kusikia, na macho yake ambayo anayatumia kuonea, na mikono yake ambayo anayatumia kushikia, na miguu yake ambayo anatumia kutembea, na anponiomba, kwa hakika ninamtakabalia, na anapotaka kinga kutoka kwangu, kwa hakika nitamkinga.<sup>29</sup>

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

بَلَىٰ مَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ وَاتَّقَىٰ فَإِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧٦﴾

Bali anaye timiza ahadi yake na akawa na taqwa basi hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wale ambao ni muttaqoon (wema na wachamngu).<sup>30</sup>

#### **14 - Taqwa inamfanya Muumini kuwa na elimu, na ndio ufunguo wa elimu.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَاتَّقُوا اللَّهَ وَيُعَلِّمُكُمُ اللَّهُ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٨٢﴾

Na kuwa na taqwa ya Allah, na Mwenyezi Mungu atakufunza, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.<sup>31 32</sup>

---

<sup>29</sup> Saheeh Bukharee

<sup>30</sup> Soorah al-Imraan 3:76

<sup>31</sup> Soorah al-Baqarah 2:282

<sup>32</sup> Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

**15 – Taqwa inamfanya Muumini kuwa na nguvu. Mtu aliye na taqwa atakingwa na kupotea njia na kuepukana na njia ilio nyoka, baada ya Mwenyezi Mungu amempa uongofu.**

Mwenyezi Mungu alietukuka amesema;

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ فَاتَّبِعُوهُ وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَنْ سَبِيلِهِ ذَٰلِكُمْ وَصَدُكُمْ بِهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٥٣﴾

Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuata njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuwa na al-muttaqoon. <sup>33</sup>

**16 – Taqwa inamfanya Muumin kupata Rehma ya Mwenyezi Mungu, na hii rehma ni ya katika maisha haya na ya kesho akhera.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema:

---

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ  
وَأَمُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِنْ رَحْمَتِهِ وَيَجْعَلْ لَكُمْ  
نُورًا تَمْشُونَ بِهِ

Enyi mlio amini! Kuweni na taqwa ya Allah, na muaminini Mtume wake, atakupeni sehemu mbili katika Rehma Yake, na atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo. [Soorah al-Hadeed 57: 28]

Enyi mlio amini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atakupeni furqaan (kipambanuo cha kujua baina ya sawa na makosa) [Soorah al-Anfaal 8: 29]

<sup>33</sup> Soorah al-An'aam 6: 153



وَرَحْمَتِي  
 وَسَعَتْ كُلَّ شَيْءٍ فَسَأَكْتُبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤْتُونَ  
 الزَّكَاةَ وَالَّذِينَ هُمْ بِآيَاتِنَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٥٦﴾

Na rehema yangu imeenea kila kitu. Lakini nitawaandikia khasa wale muttaqoon, na wanao toa Zaka, na wale ambao wanaziamini Ishara zetu. <sup>34</sup>

### 17 – Taqwa inamfanya Muumin kupata uandamano wa Mwenyezi Mungu, na hii ni kwa njia mbili:

i) Ya kwanza ni kwa waja wote, ambapo Mwenyezi Mungu anawaandama kwa Kuwasikiza, Kuwana na Kuwa na Elimu kwani Mwenyezi Mungu Alietukuka ndie Mwenye Kusikia, Kuona, na Kuyajua yote wanayoyafanya waja Wake.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ

Naye (Mwenyezi Mungu) yuko pamoja nanyi popote pale mulipo. <sup>35</sup>

Mwenyezi Mungu Alitukuka amesema;

---

<sup>34</sup> Soorah alA'raaf 7: 156

<sup>35</sup> Soorah al-Hadeed 57: 4

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَا يَكُونُ  
 مِنْ نَجْوَى ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ  
 وَلَا آدْنَى مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا

Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi? Hauwi mning'ono wa watu watatu ila Yeye huwa ni wane wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao. Wala wa wachache kuliko hao, wala walio wengi zaidi, ila Yeye yu pamoja nao popote pale walipo.<sup>36</sup>

ii) Ama ya pili, ni khususan wenye usaidizi wa Allah, neema zake na kinga.

Kama vile Mwenyezi Mungu Alietukuka alivyosema:

لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا

Wala usihuzunike, hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja nasi.<sup>37</sup>

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

قَالَ لَا تَخَافَا إِنَّنِي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَى

Naye (Mwenyezi Mungu) akasema, Usiwe na hofu, niko pamoja nanyi (Moosa na Haaron), Nasikia na Naona.<sup>38</sup>

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

<sup>36</sup> Soorah al-Mujaadalah 58: 7

<sup>37</sup> Soorah at-Tawbah 9: 40

<sup>38</sup> Soorah Taa Haa 20: 46

إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾

Kwa hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wale wenye taqwa, na wale wanaotenda mema. <sup>39</sup>

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿٣٦﴾

Najua kwa hakika kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye kumcha (muttaqeen) <sup>40</sup>

### 18 – Hakika watakuwa na marudio mema siku ya Kiyama kwa ajili ya taqwa juu ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَالْعَاقِبَةُ لِلتَّقْوَىٰ ﴿١٣٢﴾

Na mwisho mwema ni wa mwenye taqwa. <sup>41</sup>

وَإِنَّ لِلْمُتَّقِينَ لَحُسْنَ مَّآبٍ ﴿٤٩﴾

Na hakika muttaqoon (wachamngu) wanamarudio mema. <sup>42</sup>

فَأَصْبِرْ ۗ إِنَّ الْعَاقِبَةَ لِلْمُتَّقِينَ ۗ

---

<sup>39</sup> Soorah an-Nahl 16:128

<sup>40</sup> Soorah at-Tawbah 9:36

<sup>41</sup> Soorah Taa Haa 20:132

<sup>42</sup> Soorah Saad 38:49

Basi kuwa na subira, kwani marudio mema ni ya muttaqoon (wachamngu). <sup>43</sup>

**19 - Hakika inamsababisha Muumini kuwa na bishara njema katika maisha haya, kwa kuwa na ndoto njema, au kwa kupitia mapenzi na sifa ambao watu wanaokuwa nao juu yake.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema:

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿١٣﴾ لَهُمُ الْبُشْرَىٰ  
فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

Wale walioamini na wakawa wakimcha Mwenyezi Mungu, wanao bishara njema katika haya maisha ya duniya na ya kesho ya akhera. <sup>44</sup>

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa Aboo Dardaa kuwa Mtume Sallallahu Alaihi Wasalam amesema kuhusu neno la Mwenyezi Mungu;

لَهُمُ الْبُشْرَىٰ

wanao bishara njema

“Nayo ni ile ndoto njema (inayo toa bishara njema) ambayo Muislamu ataiona, au ataonekana nayo na mwту mwengine.” <sup>45</sup>

---

<sup>43</sup> Soorah Hood 11:49

<sup>44</sup> Soorah Yunus 10:63-64

<sup>45</sup> Saheeh Muslim

Aboo 'Umar al-Ghafaaree radhiallahu anhu amesema kuwa alimuuliza Mtume Sallallahu Alaihi Wasalam: "Ewe mjube wa Mwenyezi Mungu! Ni yapi kuhusu mtu ambaye anatenda mema ambayo watu wanamsifu na kumpendea?Mtume akajibu: "Hio ndio bishara njema katika maisha haya kwa Muumini".<sup>46</sup>

**20 – Taqwa inampinga mwanamke na kulegeza sauti, huko kunamsimamisha mwanamume mwenye ugonjwa katika moyo wake (yaani matamanio maovu ya kuzini).**

Mwenyezi Mungu Aalietukuka amesema;

يَدِينَسَاءَ النَّبِيِّ

لَسْتُنَّ كَأَحَدٍ مِّنَ النِّسَاءِ إِنِ اتَّقَيْتُنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ  
فَيَطْمَعَ الَّذِي فِي قَلْبِهِ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٣٧﴾

Enyi wakeze Mtume! Nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine. Kama mnamcha Mungu basi msilegeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema.<sup>47</sup>

**21 – Kwa hakika, inazuwia dhulma katika mambo ya mali na pesa (k.m. wasia, au ushahidi n.k)**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

---

<sup>46</sup> Saheeh Muslim

<sup>47</sup> Soorah al-Ahzaab 33:32

كُتِبَ عَلَيْكُمُ  
 إِذَا حَضَرَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ إِن تَرَكَ خَيْرًا الْوَصِيَّةَ لِلْوَالِدَيْنِ  
 وَالْأَقْرَبِينَ بِالْمَعْرُوفِ ۗ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿١٨٠﴾

Mumefaradhishiwa kwenu; mmoja wenu anapo fikwa na mauti, kama akiacha mali, afanye wasia kwa wazazi wake na jamaa zake kwa namna nzuri inayo pendeza. Ni waajibu haya kwa muttaqoon (wachamngu).<sup>48</sup>

**22 – Inamfanya Muumini kumpa mke alietalikiwa haki yake ya posho.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَالْمُطَلَّاتِ مَتَّعٍ بِالْمَعْرُوفِ ۗ حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِينَ ﴿٢٤١﴾

Na wanawake walio achwa wapewe cha kuwaliwaza kwa kiasi kinacho ekewa. Haya ni waajibu kwa muttaqoon (wachamngu).<sup>49</sup>

**23 – Kwa hakika inamsababisha Muumini kutokosa malipo mema aliyoyatuma, katika maisha ya hapa au ya kesho akhera.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema baada ya kumjazi Yousuf alaihi salaam na rehma Zake, kwa kumkutanisha na familia yake:

إِنَّهُ مَن يَتَّقِ وَيَصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٩٠﴾

---

<sup>48</sup> Soorah al-Baqarah 2:180

<sup>49</sup> Soorah al-Baqarah 2:241

Hakika anaye mcha Mwenyezi Mungu na akasubiri, basi Mwenyezi Mungu haachi ukapotea ujira wa wafanyao mema.  
50

## 24 – Hakika inamfanya Muumini kupata uongozi.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

آلَمْ ۙ ذَٰلِكَ ٱلْكِتَٰبُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ ۙ ٱلَّذِينَ  
يُؤْمِنُونَ بِٱلْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ۙ

Alif Laam Meem. Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uwongofu kwa wachamungu. Ambao huyaamini ya ghaibu na hushika Sala, na hutoa katika tuliyo wapa.<sup>51</sup>

أُو۟لَٰئِكَ عَلَىٰ هُدًى مِّن رَّبِّهِمْ ۗ وَأُو۟لَٰئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ۗ

Hao wapo juu ya uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, na hao ndio walio fanikiwa.<sup>52</sup>

---

<sup>50</sup> Soorah Yoosuf 12:90

<sup>51</sup> Soorah al-Baqarah 2:1-3

<sup>52</sup> Soorah al-Baqarah 2:5

## Manufaa Atakayo yapata Muumini Kwa Ajili ya Kuwa na Taqwa ya Mwenyezi Mungu.

### 1 – Inamfanya Muumini kuwa mtukufu mbele ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتَقْوَكُمْ

Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni aliye na taqwa zaidi.<sup>53</sup>

### 2 – Inamfanya Muumini kuwa ni mwenye kufaulu.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَخْشِ اللَّهَ وَيَتَّقْهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ

Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamwogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu.<sup>54</sup>

### 3 – Hakika inamwkoa Muumini na adhabu ya Mwenyezi Mungu Alietukuka, siku ya Kiyama.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَإِنْ مِنْكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا كَانَ عَلَى رَبِّكَ

حَتْمًا مَقْضِيًّا ﴿٧١﴾ ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوْا وَنَذَرُ الظَّالِمِينَ

فِيهَا جَنَّتًا ﴿٧٢﴾

<sup>53</sup> Soorah al-Hujuraat 49:13

<sup>54</sup> Soorah an-Noor 24:52



Wala hamna yeyote kati yenu ila ni mwenye kupita juu yake (moto wa Jahannam). Hiyo ni hukumu ya Mola wako Mlezi ambayo lazima itimizwe. Kisha tutawaokoa wale walio mchamngu; na tutawaacha madhaalimu humo (wakinyeyekea) wamepiga magoti (katik moto wa Jahannam).<sup>55</sup>

وَسَيُجَنَّبُهَا الْأَتْقَى ﴿١٧﴾

Na muttaqoon (wachamngu) wataepushwa nayo (Moto wa Jahannam).<sup>56</sup>

#### 4 – Inasababisha vitendo vyema vya Muumini kutakabaliwa.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ

Hakika Mwenyezi Mungu huyakubali ya wenye kumcha.<sup>57</sup>

#### 5 - Inamfanya Muumini kurithi Pepo.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

تِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي نُورِثُ مِنْ عِبَادِنَا مَنْ كَانَ تَقِيًّا ﴿١٣﴾

Hiyo ndiyo Pepo tutakayo warithisha katika waja wetu walio kuwa muttaqoon (wachamngu).<sup>58</sup>

<sup>55</sup> Soorah Maryam 19:71-72

<sup>56</sup> Soorah al-Layl 92:17

<sup>57</sup> Soorah al-Maidah 5:27

## 6 – Hakika inawafanya waaumini kuwa na vyumba vya fakhari (Peponi) moja juu ya nyengine.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

لَكِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ لَهُمْ غُرَفٌ مِّنْ فَوْقِهَا غُرَفٌ مَّبْنِيَّةٌ تَجْرِي  
مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَعَدَّ اللَّهُ لَا يُخْلِفُ اللَّهُ الْمِيعَادَ ﴿٢٠﴾

Lakini walio mcha Mola wao watapata ghorofa za fakhari zilizo jengwa juu ya ghorofa; chini yake hupita mito. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake. <sup>59</sup>

Kunayo hadeeth inayosema: Hakika katika Pepo, kunayo vyumba ambazo mbele yake inaonekana kwa nyuma, na nyuma yake yaonekana kwa mbele. Kisha mbedui mmoja akauliza: Vyumba hivyo vitakuwa vya kina nani ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Naye Salallahu Alaihi Wasallam akamjibu: "Yule anayezungumza mazuri, anayelisha masikini, na anyesali sala ya usiku (tahajjud) wakati watu wamelala." <sup>60</sup>

## 7 – Hakika itawafanya waumini kuwa na daraja za juu mbele ya makafiri siku ya Kiyama, na watakuwa na makao ya juu katika Pepo.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

---

<sup>58</sup> Soorah Maryam 19:63

<sup>59</sup> Soorah az-Zumar 39:20

<sup>60</sup> Sunan at-Tirmidhee

زُيِّنَ لِلَّذِينَ  
كَفَرُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَيَسْخَرُونَ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ  
اتَّقَوْا فَوْقَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ

Walio kufuru wamepambiwa maisha ya duniani; na wanawafanyia maskhara walio amini. Na wenye kuchamngu watakuwa juu yao Siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu humruzuku (katika Neema zake na Rehema zake Siku ya Kiyama) amtakaye bila ya hisabu.<sup>61</sup>

## 8 – Hakika itawafanya wawe ni wenye kuingia katika Pepo, na hiyo ni kwa sababu Pepo imetayarishwa kwa wale wenye taqwa.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا  
السَّمَاوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾

Na kimbilieni maghfira kutoka kwa Mola wenu, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyo tayarishiwa muttaqoon (wachamngu).<sup>62</sup>

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْكِتَابِ ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا لَكَفَّرْنَا عَنْهُمْ  
سَيِّئَاتِهِمْ وَلَأَدْخَلْنَاهُمْ جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿١٥﴾

<sup>61</sup> Soorah al-Baqarah 2:212

<sup>62</sup> Soorah al-'Imraan 3:133

Na lau kuwa Watu wa Kitabu (wakiristo na mayahudi) wangeli amini (Mtume Muhammad Salallahu Alaihi Wasallam) na wakachamngu hapana shaka tungeli wafutia makosa yao, na tungeli waingiza katika Bustani zenye neema <sup>63</sup>

**9 – Hakika inasababisha kufutwa kwa vitendo viovu na kusamehewa kwa makosa Muumini ambayo ameyafanya.**

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يُكَفِّرْ عَنْهُ سَيِّئَاتِهِ وَيُعْظِمْ لَهُ أَجْرًا ﴿٥٦﴾

Na anaye mcha Mwenyezi Mungu atamfutia maovu yake, na atampa ujira mkubwa. <sup>64</sup>

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْكِتَابِ ءَامَنُوا وَاتَّقَوْا لَكَفَّرْنَا عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَأُدْخِلَنَّهُمْ جَنَّاتٍ النَّعِيمِ ﴿٦٥﴾

Na lau kuwa Watu wa Kitabu (wakiristo na mayahudi) wangeli amini (Mtume Muhammad Salallahu Alaihi Wasallam) na wakachamngu hapana shaka tungeli wafutia makosa yao, na tungeli waingiza katika Bustani zenye neema. <sup>65</sup>

**10 – Hakika inamfanya Muumini kupata kila moyo wake unaotamani, na kile kinachomridhisha kwa macho yake.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

---

<sup>63</sup> Soorah al-Maaidah 5: 65

<sup>64</sup> Soorah at-Talaaq 65: 5

<sup>65</sup> Soorah al-Maa'idah 5: 65

جَنَّتٍ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ لَهُمْ فِيهَا  
 مَا يَشَاءُونَ كَذَلِكَ يَجْزِي اللَّهُ الْمُتَّقِينَ ﴿٣١﴾

Bustani za milele wataziingia; inayopita chini yake  
 mito. Humo watapata watakacho. Hivi ndivyo  
 Mwenyezi Mungu awalipavyo muttaqoon  
 (wachamngu). <sup>66</sup>

### 11 – Hakika, itamfanya Muumini kutogopa wala kutohuzunika, wala hamna shari yeyote itakayowafikia siku ya Kiyama.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَيُنَجِّي اللَّهُ الَّذِينَ اتَّقَوْا  
 بِمَقَازَتِهِمْ لَا يَمَسُّهُمُ السُّوءُ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦١﴾

Na Mwenyezi Mungu atawaokoa wenye taqwa  
 (wachamngu), kwa mahali pao pa kufuzu (Peponi).  
 Hapana uovu utao wagusa, wala hawatahuzunika. <sup>67</sup>

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفَ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ

Bila Shaka! Hakika awliyaa' (marafiki) wa Mwenyezi  
 Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika. <sup>68</sup>

<sup>66</sup> Soorah an-Nahl 16:31

<sup>67</sup> Soorah az-Zumar 39:61

<sup>68</sup> Soorah Toonus 10:62

**12 – Watakusanywa siku ya Kiyama, wafdan (kama mgeni aliemuelekea mfalme alietukuzwa) na maana ya wafdan ni kuwa watamjia Mwenyezi Mungu Alietukuka, kwa vipando.**

يَوْمَ نَحْشُرُ الْمُتَّقِينَ إِلَى الرَّحْمَنِ وَفْدًا

Siku tutakayo wakusanya muttaqoon (wachamngu) kuwapeleka kwa Mwingi wa Rehema kuwa ni (wafdan) wageni (mbele ya Mfalme Alietukuzwa).<sup>69</sup>

Ibn Katheer amesema, huku akinukuu hadeeth ilotolewa na Nu'maan ibn Sa'eed kuwa amesema; "Tulikuwa tumekaa na 'Alee radiallaahu-anhu wakati 'Alee akaisoma aayah hii, "Siku tutakayo wakusanya muttaqoon (wachamngu) kuwapeleka kwa Mwingi wa Rehema kuwa ni (wafdan) wageni (mbele ya Mfalme Alietukuzwa)" Akasema, "La, naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, hawatakusanywa huku wamesimama na miguu yao. Hao wageni hawatakusanywa huku wamesimama na miguu yao, bali watakuwa wamepanda ngamia w akike, mfano wake hamna kiumbe ameuona, (saddles) zao zimetengenezwa na dhahabu, watapanda vpando hivo mpaka watakapobisha katika milango ya Peponi."

**13 – Pepo itasongezwa karibu yao, kwa ajili ya kuwa na taqwa.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

وَأَزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِينَ

Na Pepo itasogezwa karibu na muttaqoon (wachamngu).<sup>70</sup>

---

<sup>69</sup> Soorah Maryam 19:85

**14 – Hakika itamfanya Muumini kutokuwa daraja moja na ma fujjaar (waovu, wakosi) au ma kuffaar (makafiri).**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

أَمْ نَجْعَلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ  
كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ كَالْفُجَّارِ ﴿٢٨﴾

Tuwafanye walio amini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu na ufisadi katika nchi? Au tuwafanye muttaqoon (wachamngu) kama ma fujjaar (waovu, na wakosi)?<sup>71</sup>

**15 – Kila aina ya ushuba au urafiki ambao uliokuwa na mwengine asiyekuwa Mwenyezi Mungu utageuzwa siku ya kiyama kuwa ni uadui, isipokuwa ushuba wa wale waliokuwa na taqwa.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

الْأَخِلَاءُ يَوْمَئِذٍ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ إِلَّا الْمُتَّقِينَ ﴿٢٧﴾

Siku hiyo marafiki watakuwa ni maadui, wao kwa wao, isipo kuwa muttaqoon (wachamngu).<sup>72</sup>

---

<sup>70</sup> Soorah ash-Shu'araa 26:90

<sup>71</sup> Soorah Saad 38:28

<sup>72</sup> Soorah az-Zukhruf 43:67

**16 – Watakuwa katika sehemu za amani, miongoni mwa bustani na mibwoji (chemchem za maji).**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي مَقَامٍ أَمِينٍ ﴿٥١﴾ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ  
يَلْبَسُونَ مِنْ سُندُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ مُتَقَابِلِينَ ﴿٥٢﴾  
كَذَلِكَ وَزَوَّجْنَاهُمْ بِحُورٍ عِينٍ ﴿٥٣﴾ يَدْعُونَ فِيهَا  
بِكُلِّ فَاكِهَةٍ آمِنِينَ ﴿٥٤﴾ لَا يَذُقُونَ فِيهَا الْمَوْتَ  
إِلَّا الْمَوْتَ الْأُولَىٰ ۗ وَوَقَّعَهُمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ ﴿٥٥﴾

Hakika muttaqoon (wachamngu) watakuwa katika mahali pa amani (Peponi). Katika mabustani na chemchem (mibwoji). Watavaa hariri nyepesi na hariri nzito wakikabiliana. Hivi ndivyo itakavyo kuwa, na tutawaoza mahurilaini. Humo watataka kila aina ya matunda, na wakae kwa amani. Hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza (ya duniyani), na (Mwenyezi Mungu) atawalinda na adhabu ya Jahannamu.<sup>73</sup>

**17 – Hakika watakuwa na makalio ya haki (Peponi) karibu na Mfalme alie Jabari, Mwenyezi Mungu Alietukuka.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

فِي مَقْعَدٍ صِدْقٍ عِنْدَ مَلِيكٍ مُّقْتَدِرٍ ﴿٥٥﴾

<sup>73</sup> Soorah ad-Dukhaan 44:51-56



Katika makalio ya haki (Peponi) kwa Mfalme Jabari (Mwenye uweza).<sup>74</sup>

**18 – Taqwa ni njia ya kuwa na mito tofauti Peponi, mto wenye maji matamu, mwengine wa maziwa ambayo haiharibiki ladha yake, na mto wa mvinyo, tamu kwa wanywao.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

مَثَلُ الْجَنَّةِ  
الَّتِي وَعَدَ الْمُتَّقُونَ فِيهَا أَنْهَرٌ مِنْ مَاءٍ غَيْرِ آسِنٍ وَأَنْهَرٌ مِنْ لَبَنٍ لَمْ  
يَتَغَيَّرَ طَعْمُهُ وَأَنْهَرٌ مِنْ خَمْرٍ لَذَّةٍ لِلشَّرِيبِينَ وَأَنْهَرٌ مِنْ عَسَلٍ مُصَفًّى  
وَلَهُمْ فِيهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَمَغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ

Mfano wa Pepo walioahidiwa muttaqoon (wachamngu) ina mito ya maji yasiyo vunda, na mito ya maziwa isiyo haribika ladha yake, na mito ya mvinyo yenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali iliyo safishwa. Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda, na maghfira kutoka kwa Mola wao Mlezi.<sup>75</sup>

Inapatikana hadeeth katika Saheeh ya Bukharee ambayo Mtume Salallahu Alaihi Wasallam amesema; “Munapomwomba Mwenyezi Mungu Alietukuka, basi mwombeni (Pepo iitwayo) al-Firdous, kwani, imo katikati ya Peponi, na ndio daraja ya juu zaidi katika Pepo ambapo mito yanatiririka, na juu yake ni arshi ya Mwingi wa Rehma (Allah).”

---

<sup>74</sup> Soorah al-Qamar 54:55

<sup>75</sup> Soorah Muhammad 47:15

**19 – Taqwa inamfanya Muumini kuwa na uwezo wa kusafiri chini ya vivuli vya miti ya Peponi, na kuburudika chini ya vivuli hivo.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي  
ظِلِّ وَعُيُونٍ ﴿٤١﴾ وَفَوَاحِهِ مِمَّا يَشْتَهُونَ ﴿٤٢﴾  
كُلُوا وَأَشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٣﴾

Hakika wachamngu watakuwa katika vivuli na chemchem. Na matunda wanayo yapenda. Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa yale mliyo kuwa mkiyatenda. <sup>76</sup>

Anas bin Maalik radiallaahu-anhu amesema kuwa Mtume Salallahu Alaihi Wasallam amesema: "Hakika ndani ya Pepo, kuna mti ambao mrakibu atasafiri chini ya kivuli chake kwa masafa wa miaka mia na asiupite mwisho wake." <sup>77</sup>

**20 – Kwa wenye taqwa, siku ya Kiyama watakuwa na bishara njema, misukosuko (ya Siku hio ya Kiyama) haitawahuzunisha, na watakutana na malaika.**

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

---

<sup>76</sup> Soorah al-Mursalaat 77: 41-43

<sup>77</sup> Saheeh Bukharee

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٣﴾  
 الَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿١٣﴾ لَهُمُ الْبُشْرَىٰ فِي الْحَيَاةِ  
 الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

Bila Shaka! Awliyaa (marafiki) wa Mwenyezi Mungu hawatafikwa na khofu wala hawatahuzunika. Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu (kwa kujiepusha na vitendo viovu na dhambi na wakafanya vitendo vyema). Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. <sup>78</sup>

Ibn Katheer amesema: "Ama kuhusu bishara njema siku ya Akhera, ni yale aliosema Mwenyezi Mungu Alietukuka;

لَا يَحْزَنُهُمُ الْفَزَعُ الْأَكْبَرُ وَتَتَلَقَّيْنَهُمُ  
 الْمَلَائِكَةُ هَذَا يَوْمَ كُمْ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿١٠٣﴾

Hicho kitisho kikubwa (cha Siku ya Kiyama) hakito wahuzunisha. Na Malaika watawapokea (kwa kuwaambia): Hii ndiyo Siku yenu mliyo kuwa mkiahidiwa! <sup>79</sup>

## 21 – Hakika, muttaqoon watakuwa na makazi mema siku ya Akhera.

Mwenyezi Mungu Alietukuka amesema;

<sup>78</sup> Soorah Yoonus 10:62-64

<sup>79</sup> Soorah al-Ambiyaa 21:103

وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ وَلَنِعْمَ دَارُ الْمُتَّقِينَ

Na nyumba ya Akhera ni bora zaidi, na njema mno nyumba ya muttaqoon (wachamngu). <sup>80</sup>

**22 – Hakika wenye taqwa watakuwa na malipo yao, na vitendo vyao vyema vitaongezwa, kama Mwenyezi Mungu Alietukuka alivyosema.**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنقُوا اللَّهَ  
وَءَامِنُوا بِرَسُولِهِ ءُؤْتِكُمْ كَفْلَيْنِ مِن رَّحْمَتِهِ ءُ وَيَجْعَل لَّكُمْ  
نُورًا تَمْشُونَ بِهِ ءُ

Enyi mlio amini! Kuweni na taqwa ya Allah, na muaminini Mtume wake, atakupeni sehemu mbili katika Rehma Yake, na atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo. <sup>81</sup>

Tunamwomba Mwenyezi Mungu Alietukuka atujaalie sisi miongoni mwa waja wake wenye taqwa na wenye shukrani. Sifa zote njema ni zenye kumthubutukia Allah, Mola wa ulimwengu. Na swala Zake na salamu zimfikie Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Muhammad Sallallahu Alaihi Wasalam, na jamii yake, na maswahaba zake.

---

<sup>80</sup> Soorah an-Nahl 16:30

<sup>81</sup> Soorah al-Hadeed 57:28